

Maswali

1. Mungu alimwambia Yona afanye nini?
2. Mbona Yona hakutaka kwenda Ninawi?
3. Yona alifanya nini?
4. Yona alitoka akaenda wapi?
5. Ni nini ilifanyika kwa meli yenye Yona alikuwemo?
6. Mabaharia walimfanyaje Yona?
7. Mungu alimuokoa Yona namna gani kutoka kwa bahari?
8. Yona alitokaje kwa samaki?
9. Mungu alimwambia Yona afanye nini?
10. Watu wa Ninawi waliomba msamaha?

Majibu

1. Mungu alimwambia Yona aende Ninawi
2. Yona hakutaka kuenda Ninawi kwa sababu hao watu walikuwa maadui
3. Yona alitoroka
4. Yona alienda Yafa kwa bahari
5. Meli iliyokuwa imebeba Yona ilikuwa karibu kuzama kwa ajili ya dhoruba
6. Mabaharia walitupa Yona baharini
7. Yona aliokoka kwa sababu Mungu alifanya samaki ikammeza
8. Yona alitoka kwa samaki kwa sababu Mungu alifanya samaki ikawa mgonjwa
9. Mungu alimwambia Yona aende Ninawi
10. Watu wa Ninawi waliomba msamaha

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

30 Yona

Marejeo

Yona

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba ni lazima kumtii Mungu kila siku


Maneno maalum

1. Mungu + Yona + Ninawi + toroka
2. Upepo + dhoruba + mabaharia + meli
3. Ogopa + tupa + bahari + tuliza
4. Samaki mkubwa + meza + omba
5. Siku arobaini + haribu + okoka + jiji


30.1 Mungu alimwambia Yona aende kwa mji mkubwa wa Ninawi. Lakini Yona hakutaka kuenda Ninawi. Yona alijua kwamba mfalme wa nguvu anayeishi huko atakuja kupiga watu wake. Kwa hivyo Yona alitoroka, akaenda Yafa iliyokuwa karibu na bahari. Alipata meli iliyokuwa ikienda mbali sana. Alilipa nauli na akaingia kwa meli na ikaondoka ikaenda.

30.2 Lakini Mungu alituma upepo uliokuwa na dhoruba kubwa. Upepo ulivuma na bahari ikachafuka na meli ilielekea kuzama. Mabaharia wote waliogopa, wakatuba mizigo baharini, wakijaribu kuokoa meli. Yona aliyekuwa amechoka kwa ajili ya safari yake alikuwa analala.

Nahodha wa meli akamwendea Yona na kumuuliza, “Mbona unalala? Unajua kwamba meli iko inazama? Omba Mungu wako atuokoe.” Kwa vile Yona alikuwa ameambia mabaharia wenzake kwamba anatoroka kutoka kwa Mungu, walimuendea. Wakamuuliza, “Mbona tuna pata hii shida? Umfanyia nini Mungu hata akatukasirikia?” Alijibu, “Mimi ni Mwebrania, ninaabudu Bwana Mungu wa mbinguni aliyefanya bahari na nchi kavu.”



30.3 Mabaharia waliposikia Yona akisema hivyo, waliogopa zaidi wakamuuliza, “Tukufanyeje ndio bahari itulie tena?” Yona akasema, “Nichukue mnitupe baharini halafu itatulia.” Kwa hivyo walimchukua Yona wakamtupa baharini na bahari ikatulia tena.



30.4 Yona alizama ndani ya bahari kabisa. Akafikiria atapotea lakini Mungu alikuwa ametuma samaki mkubwa kummeza. Alipokuwa akiingia ndani ya maji, samaki ilifungua mdomo wake na kummeza Yona. Alikaa ndani ya samaki siku tatu usiku na mchana, akaomba Mungu amuokoe. Mungu alizungumzia samaki ikaogelea mpaka ukingoni na ikawa mgonjwa. Ilipokuwa hapo kando, Yona alitoka kwa samaki. Mungu alimwambia Yona, “Enda Ninawi upeleke ujumbe niliokupa.”

30.5 Kwa hivyo Yona alienda Ninawi. “Kwa siku arobaini Ninawi itaangamishwa,” alipaza sauti alipokuwa akitembea jijini. Watu wa Ninawi walisadiki ujumbe kutoka kwa Mungu na wakaomba msamaha. Mungu aliwasamehe na kuwambia kwamba hata liangamiza jiji la Ninawi.